

Je, unaweza kufa ukitumia dawa za kulevya?

By SW - Melkisedeck Shine · April 17, 2022

Ujana na Makuzi | Mapenzi na Ngono Salama

Ndiyo, unaweza. Kifo kinaweza kuwa cha ghafla au kutokana na madhara ya muda mrefu katika viungo vya ndani ya mwili kutokana na matumizi ya dawa za kulevya. Watu wengi hufa katika ajali pale wanapokuwa wana kiasi kikubwa cha kilevi katika damu, kwani wanashindwa kutambua mazingira ya hatari. Mtumiaji wa dawa za kulevya anaweza akafa ghafla kwa kile kinachoitwa kuzidisha dawa, pale mtu atakapotumia dawa za kulevya zaidi ya uwezo wa mwili. Kifo cha ghafla kinaweza kutokea au kutokana na matumizi ya kokaini na vifukishi kama petroli bila hata ya kuzidisha kiwango. Watumiaji wa vifukishi kama petroli mara nyingi hutumia mifuko ya plastiki ili kuongeza kiwango cha mvuke wanaovuta. Katika mazingira haya ni rahisi kupoteza fahamu kutokana na kukoseshwa hewa na mifuko hiyo. Kuchanganya baadhi ya dawa za kulevya kama vile heroini na dawa zingine hasa dawa za kutuliza maumivu (mfano valium) au pombe pia huweza kusababisha kifo.

Printable AckySHINE Article · <https://ackyshine.com/post.php?post=25775>